THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**121/2** **KISWAHILI 2**
**(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)**

*Muda: Saa 3* *Jumatano 13 Februari 2008 asubuhi*

---

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali matano (5) kwa kuchagua swali moja kutoka kila sehemu.
3. Simu za mkononi haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
4. **Andika Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## FASIHI KWA UJUMLA

1. Fasihi Simulizi inaathiriwa kwa kiasi kikubwa na utandawazi. Jadili kauli hii kwa kutoa mifano halisi.

2. Fasihi ni sawa na kinyonga. Jadili kauli hii ukitumia utanzu wa riwaya ya Kiswahili.

3. Msanii na mhakiki ni watu wanaotegemeana katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Thibitisha kauli hiyo.

## SEHEMU B (alama 20)

## USHAIRI

| | |
|---|---|
| **Kimbunga** | - H. Gora |
| **Mapenzi Bora** | - S. Robert |
| **Chungu Tamu** | - T.A. Mvungi |
| **Wasaka Tonge** | - M.S. Khatib |

4. Mshairi si mzushi wa mambo bali ni mchambuzi wa masuala ya jamii. Jadili hoja hiyo kwa kutumia vitabu **viwili (2)** vya ushairi kati ya vilivyoorodheshwa.

5. Jadili dhamira ya usaliti na utengano kama ilivyojitokeza katika kazi za washairi **wawili (2)** ulizosoma.

6. Kwa kutumia vitabu **viwili (2)** ulivyosoma thibitisha kuwa mashairi yanaburudisha na kuelimisha jamii.

## SEHEMU C (alama 20)

## RIWAYA

| | |
|---|---|
| **Janga Sugu la Wazawa** | - Gabriel Ruhumbika |
| **Barua Ndefu Kama hii** | - Mariama Ba |
| **Pesa Zako Zinanuka** | - Ben R. Mtobwa |
| **Vuta N'kuvute** | - Shafi Adam Shafi |

7. Teua riwaya **mbili (2)** kati ya zilizoorodheshwa na ueleze jinsi kipengele cha muundo kinavyotofautisha kazi za wasanii wa riwaya hizo.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

8. Jadili dhamira ya utu kama ilivyojitokeza katika riwaya mbili (2) ulizosoma.

9. Jadili uhalisia wa riwaya mbili (2) ulizosoma.

## SEHEMU D (alama 20)

## TAMTHILIYA

| | |
|---|---|
| **Kwenye Ukingo wa Thim** | - E. Hussein |
| **Morani** | - E. Mbogo |
| **Kivuli Kinaishi** | - S. Mohamed |
| **Nguzo Mama** | - P. Muhando |

10. Wanaume ni kikwazo kikubwa sana katika maendeleo ya mwanamke katika jamii. Kubali au kataa kauli hiyo kwa kutumia tamthiliya **mbili (2)** ulizosoma kati ya hizo zilizotajwa.

11. Mitindo waitumiayo wasanii katika kuziunda tamthiliya, hufanya tamthiliya moja iwe imefanikiwa vizuri zaidi kufikisha ujumbe kuliko nyingine. Kwa kutumia tamthiliya **mbili (2)** ulizosoma thibitisha ukweli huo.

12. **Kazi nyingi za fasihi andishi katika jamii yetu zimekumbwa na wakati, hivyo haziwezi kuleta mabadiliko yoyote. Kwa kutumia tamthiliya mbili (2) ulizosoma kubali au kataa hoja hiyo.**

## SEHEMU E (alama 20)

## USANIFU WA MAANDISHI

13. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.

Mtu wa fikra njema na kwa watu huacha jina,
Na watu waja nyuma wakapenda kulisoma,
Katika dunia nzima likawa kubwa hazina,
Kwa kujua jambo jema lisilokuwa na <u>shari,</u>
Mvuka nguo <u>chutama</u> wendapo wajihadhari.

Na busara ni kutenda tendo ambalo ni jema,
Viumbe wakalipenda ukapata na heshima,
<u>Tabasuri</u> na <u>hikima</u> ni muhimu maishani,
Maisha daima yenda, utaacha nini nyuma?



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Ni roho yenye hekima, usambe ni santuri,
Ambayo huweza sema maneno kwa <u>kukariri,</u>
Hali haina uzima, ufahamu na tafakuri.

Kama akili hunena tungeshindwa na vinanda,
Ya sauti nzuri sana, vinavyoweza kutenda,
Fikra ni fani bora, katika fani za watu,
Waledi wenye busara na maarifa ya vitu,
Wanafahamu kwa sura, ulimwengu wetu wote

Hekima na busara ya mtu,
Hupimwa kwa matendo mema,
Ayatendayo yenye utii,
Na wala si maneno mengi kinywani

MASWALI

(a) Andika kichwa cha shairi hili

(b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili.

(c) Neno jina lina maana gani katika shairi hili?

(d) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.

14. Soma habari hii kisha eleza mbinu za kifani zilizotumika.

Malyangu, Katibu Mkuu wizarani, mwanamapinduzi, alijiona kuwa umma umekubali kumpokea. Akaanza kujisifu kuwa kati ya makatibu wakuu wote nchini yeye peke yake ndiye aliyejua shida halisi za watu. "Adhaniaye amesimama aangalie asianguke". "Adabu ni kuwa Mzee hanikumbuki." Alizoea kusema na msemo huu huwa ni dalili ya kutoridhika na cheo alichokuwa nacho mtu na huwa chanzo cha kununuliwa. Huyu ndiye alikuwa Malyangu-Paka shume ofisini, kigogo mtaani. Je nyumbani kwake? Nyumbani kwake alikuwa simba. Ule ucheshi wa ofisini hakuuonesha kwa watoto wake saba aliokuwa nao nyumbani.

Alikuwa ametoa amri, binti zake wawe wamerudi nyumbani saa kumi jioni na wasitoke tena. "Mkuki mtamu kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu". Alikuwa kigogo kwa mabinti za wenzake lakini kwa binti zake mkali kama pilipili. Kila siku asubuhi watoto wake hupita mbele yake na kutoa shikamoo ya unyenyekevu. Jioni kabla ya kulala, watoto hupita tena mbele yake na kutoa alamsiki. Yeye akiwa amekaa kwenye kochi, hutingisha kichwa kama mtemi asiyejua kusoma na kusema asante.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Wakati wa kula, Katibu Mkuu, Malyangu alizoea kukohoa – siyo kikohozi cha ugonjwa bali kile kikohozi kilionesha uzito. Kohoa yake iliitikiwa na mabinti na mchwa waliokuwa wanakula majani makavu karibu na nyumba yake kwa mlio wa ewaa! Labda alizoea kukohoa wakati wa kula ili kuwajulisha wanyonge kuwa anakula mali yake. Alikuwa hali cha kuiba. Ama kweli, "Mwenye chake ni muungwana".

Akiwa nyumbani aliweza kuzungumza na mkewe tu. Labda kweli, "Aibu ya maiti aijuaye mwosha." Utasikia akimwita mkewe, "Klotilda" na alivyojua kuziremba hizo "t" mdomoni. Hata hivyo ingawa alizungumza na mkewe, mara nyingi alikuwa na majibu ya jeuri na ya mkato. Mke alimwambia, "Baba Levina, acha kula mali ya umma! Tufafungwa!" Yeye atamjibu, "Ninaweza kula kuku mzima peke yangu itakuwa ----" Klotilda akimwambia, "Zee zima, cheo kikubwa, bado unahanjahanja mitaani." Naye Katibu Mkuu kama aliyejua alikuwa na jibu lake mdomoni, "Mwanaume huachana na uta wake kaburini." Halafu kimya. "Niletee bia." Alitoa amri bila kumtazama.

Malyangu Katibu Mkuu, ofisini pake paka shume, mitaani kigogo, nyumbani simba. Vipi mkewe?

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org